JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI
CHAMA CHA HAKIMILIKI CHA TANZANIA
Ofisi: Barabara ya Chato, Kiwanja Namba 271, Regent Estate, Mikocheni, Kinondoni
"USAJILI" S. L.P 6388, ***DAR ES SALAAM.*** *Simu: +255 22 2700019 / 0786 464007*
Barua pepe: cosotatanzania@gmail.com/ info@cosota.go.tz , Tovuti: http://www.cosota.go.tz

Barua zote ziandikwe kwa Mtendaji Mkuu:

COSOTA
COPYRIGHT SOCIETY OF TANZANIA

MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KUOMBA UANACHAMA WA COSOTA

1. ADA ZA KUOMBA UANACHAMA KWA MTANZANIA

Mtu binafsi:		Kikundi/kampuni/Kwaya/Bendi	
Ada ya Fomu	Tshs. 10,000/=	Ada ya Fomu	Tshs. 20,000/=
Ada ya Mwaka	Tshs. 20,000/=	Ada ya Mwaka	Tshs. 80,000/=
JUMLA	**Tshs. 30,000/=**	**JUMLA**	**Tshs. 100,000/=**

2. ADA ZA KUOMBA UANACHAMA KWA ASIYE MTANZANIA

Mtu binafsi:		Kikundi/kampuni/Kwaya/Bendi	
Ada ya Fomu	Tshs. 20,000/=	Ada ya Fomu	Tshs. 40,000/=
Ada ya Mwaka	Tshs. 20,000/=	Ada ya Mwaka	Tshs. 80,000/=
JUMLA	**Tshs. 40,000/=**	**JUMLA**	**Tshs. 120,000/=**

3. USAJILI WA KAZI ZA NDANI (KWA RAIA WA TANZANIA)

Usajili wa kazi (muziki, filamu, uchoraji, uchongaji, mashairi, scripts)	Tshs. 1,000/=
Maombi ya Clearance Certificate	Tshs. 10,000/=
Kusajili mifumo "software system"	Tshs. 10,000/=
Kusajili kitabu "all type of books"	Tshs. 10,000/=
Kusajili Tamasha, Tukio "events" Tv program	Tshs. 5000/=

4. USAJILI WA KAZI ZA NJE (KWA ASIYE RAIA WA TANZANIA)

Usajili wa kazi (muziki, filamu, uchoraji, uchongaji, mashairi,scripts)	Tshs. 5,000/=
Maombi ya Clearance Certificate	Tshs. 20,000/=
Kusajili mifumo "software system"	Tshs. 20,000/=
Kusajili kitabu "all type of books"	Tshs. 20,000/=
Kusajili Tamasha, Tukio "events" Tv program	Tshs. 15000/=

5. ADA NYINGINE

Kusikiliza mgogoro kila upande	Tshs. 10,000/=
Kutafuta au kuhakiki Jina la kazi kwenye mfumo (searching)	Tshs. 10,000/=
Kuomba kutafutiwa nakala ya kazi au CD	Tshs. 15,000/=
Kuomba nakala ya Barua ya usajili au "Copyright Clearance Certificate"	Tshs. 10,000/=
Kuulizia Mirabaha (pesa) migao ya nyuma zaidi ya miaka 3	Tshs. 5000/=
Kumaliza shauri na malipo kufanyika COSOTA	**5%** kila upande
Kuomba nakala ya fomu na nyaraka kwenye jalada lako	Tsh. 1,000/=

VIAMBATANISHO WAKATI WA USAJILI WA MWANACHAMA

1. **MTU BINAFSI**
   i. Picha ndogo (passport size) mbili,
   ii. Cheti cha kuzaliwa na/au nakala ya kitambulisho,
   iii. Majina/jina la mrithi wako wa baadaye (next of kin), pamoja na picha yake ndogo (passport size), nakala ya kitambulisho au Cheti cha kuzaliwa au passport,
   iv. Taarifa za benki (namba ya akaunti, tawi n.k),
   v. Mawasiliano (namba za simu, email, post address).

2. **KIKUNDI/KWAYA/KAMPUNI/BENDI**
   i. Majina ya Wanachama wa kikundi na Wawakilishi wao ikiwa ni Kikundi/Bendi/Kwaya au Kampuni.
   ii. Picha zao (passport size) za Wanachama wa Kikundi/Bendi/Kwaya au Kampuni.
   iii. Nyaraka za kikundi/kwaya/kampuni/bendi kama vile, Leseni Ya Biashara, Tra Tin Number, BRELA Registration Certificate, Memorandum And Articles Of Association (Kampuni) Katiba (Kwaya, Bendi, Kikundi), Cheti cha Usajili Basata/ Ofisi ya Utamaduni.

MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI KUSAJILI KAZI/ KULIPWA MIRABAHA.

1. Mwombaji sharti amiliki kazi inayolindwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki (Na. 7/1999).
2. Ili kuweza Kusajili kazi/kulipwa mirabaha ni sharti kuwa Mwanachama hai.
3. Aliyewahi kuwa Mwanachama kabla ya 2005/06 atapaswa kulipia uanachama (ada) wake kuanzia 2005/06.
4. WAKATI WA KUSAJILI KAZI NI SHARTI KUAMBATANISHA NAKALA MBILI ZA CD/DVD/CASSETTE NK ZA KILA ALBUM/FILAMU KWENYE KASHA GUMU "**HARD COVER**".

5. **KWA KAZI ZA MAANDISHI LETA RIGHTER UP FORM/MANUSCRIPT AU KITABU NAKALA MBILI**.
   - Writer up form/ Wazo lililoelezewa kimaandishi,
     - Utangulizi (Background)
     - Malengo (Objectives)
     - Mtiririko (Content)
     - Mwisho (Conclusion)
     - Quotations/references very important in Books.

6. **TELEVISION SHOW AND LIVE SHOW CONCERT/EVENT.**
   - Ambatanisha cd kwenye kasha gumu "hard cover" ya mfano wa kipindi (demo) nakala mbili. Kutokana na "concept" nyingi za vipindi vya televisheni kufanana, "Demo" ni muhimu kutofautisha mtiririko wa kipindi kimoja na kile kingine chenye mtiririko unaoelekea kufanana.
   - Ambatanisha DVD ya event ambayo tayari imeshafanywa.

7. **USAJILI WA COMPUTER PROGRAMS/SOFTWARE/DATABASE/SYSTEMS;**
   - Ambatanisha SOURCE CODE CD, A SYSTEM REQUIREMENT SPECIFICATION (Mahitaji Maalumu ya Mfumo), A SYSTEM DESIGN DOCUMENT (Muundo na jinsi Mfumo utakavyokuwa) na PROPOSAL inayoelezea ni jinsi gani program yako inafanya kazi.

8. Iwapo kazi unayokusudia kuisajili na kuimiliki, wewe si mtunzi halisi lakini umepata umiliki kutokana namakubaliano kati ya pande mbili, basi ni muhimu uambatanishe mkataba/mikataba sahihi inaayoonyesha ni jinsi gani upande mmoja unaweza kutumia au kumiliki kazi ya upande mwingine.

9. Kazi ya kikundi/Kwaya/Bendi au kampuni: kampuni au kikundi si mtunzi halisi, ila mara nyingi kuna Muumbaji/Wauumbaji wa wazo/Mtunzi/Mwalimu/Watunzi wa maneno/Mpangiliaji wa maneno/Sauti au vyombo, kwa makubaliano maalumu ya kulipwa kamisheni/Kujitolea/Huduma au chini ya Ajira na kikundi au kampuni husika/Tafadhali njoo na makubaliano ya kimaandishi yanayohalalisha Kikundi/Kwaya/Bendi au kampuni kumiliki ubunifu wa mtu binafsi na Washiriki wengine (kuwepo na maandishi kuhusu umilikishaji wa kazi ya mtu binafsi kwa kikundi au kampuni).

10. Njoo na mikataba ya Msambazaji/Wasambazaji wako, Mzalishaji/Wazalishaji (Producers) wako, Watangazaji wa kazi yako kwa umma (Publishers), Waongozaji/kwa ajili ya ushaidi baadaye pale inapohitajika.

11. **MALIPO YA ADA YA UANACHAMA NA USAJILI WA KAZI**

YANAFANYIKA KWA NJIA YA SIMU

UNATENGENEZEWA KUMBUKUMBU NAMBA YA MALIPO HALAFU UNALIPIA KUPITIA SIMU YAKO YA MKONONI

Siku Za Kufanya Usajili Wa Wanachama Na Kazi Zao Ni Jumatatu hadi Ijumaa Kuanzia Saa Moja Na Nusu Asubuhi (1:30) Saa Tisa Na Nusu Jioni (9:30).

12. Wakati wa kukagua kazi uloiwakilisha COSOTA, COSOTA inaweza kukuagiza kupanua wigo, kuonyesha ubunifu zaidi wa kimaandishi, kuleta nyaraka, vielelezo vya kuona na kusikia (Audio or Audiovisual) au vyote kwa pamoja ili kuweza kuleta maana kamili ya kibunifu "expression of thought or idea" au kuonyesha uhalisia wa kibunifu au ubunifu baada ya kutekeleza au kufanya kwa vitendo kwa maana ya kufanyia kazi wazo lako. COSOTA itatoa muda (specific period) wa mwezi mmoja (1 month) kuanzia tarehe ya barua ya maelekezo hayo kukabidhi nyaraka au vielelezo muhimu kuthibitisha mtiririko wa kibunifu katika dawati la usajili. Maagizo haya yote yatolewe kwa maandishi.